



## Je, unajua kuhusu uchunguzi wa bila malipo wa saratani ya matiti?

Saratani ya matiti ndiyo saratani inayogunduliwa zaidi miongoni mwa wanawake.

Kama wewe ni mwanamke aliye na umri wa miaka 40 au zaidi, unastahili kufanyiwa uchunguzi wa bila malipo wa matiti wa mamogramu (Eksirei ya matiti) kwa kutumia BreastScreen SA kila baada ya miaka miwili.

Mamogramu ya uchunguzi kwa sasa ndio njia pekee iliyodhibitishwa ya kikliniki ya kugundua saratani ya matiti mapema, kabla ya dalili kuanza kujionyesha.

Kima cha kupona cha saratani ya matiti kinazidi kuboreshwa kila mwaka, lakini ugunduzi wa mapema wa saratani ya matiti ni muhimu sana kwa matibabu rahisi na yenye ufanisi zaidi.

Afya nzuri inafaa kuwa ndio zingatiao lako la kwanza.

Miadi katika mojawapo ya kliniki zetu huchukua dakika 10 tu na wafanyakazi wetu wa kike pamoja na wataalamu wa radiografu watahakikisha kwamba unapitia katika hali tulivu iwezekanayo.

Ili kuweka miadi au kupata kujua taarifa zaidi, tupigie simu katika 13 20 50. Huduma za bila malipo za mkalimani zinapatikana endapo utazihitaji.

BreastScreen SA  
SA Health  
Telephone: 13 20 50  
[www.sahealth.sa.gov.au/breastscreen](http://www.sahealth.sa.gov.au/breastscreen)  
[BSSAenquiries@health.sa.gov.au](mailto:BSSAenquiries@health.sa.gov.au)



Government  
of South Australia

SA Health